



**AFYA**  
Serikali kulipa deni la Sh30b huku mpango wa kuhamia kwa hazina mpya ya afya ukiendelea **UK 3**



**LEBA**  
Serikali yazindua mpango kuboresha hali ya wafanyakazi wa sekta ya kibinafsi **UK 23**

**ELIMU**  
Viongozi wa duania nzima waungana kuhaikisha chakula shuleni kwa kila mtoto ifikapo 2030

# MyGov.

www.mygov.go.ke

Novemba 5, 2024

Toleo La. 19/2024-2025



Page 25

## Wakenya 13m wamesajiliwa kwa mpango mpya wa SHA

Waziri wa Afya Dkt. Deborah Barasa anasema kwamba kati ya jumla ya watu waliosajiliwa kwa mpango mpya wa SHA, karibu 7.2 milioni walihama kutoka kwa Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF), ilhali 6.2 milioni ni wanachama wapya.

NA **DOUGLAS NAMUNANE** (PCO)

**W**akenya karibu milioni 13 walikuwa wamejiandikisha katika Mamlaka mpya ya Afya ya Jamii (SHA) kufikia Oktoba 31, 2024. Akitoa tangazo hilo, Waziri wa Afya Dkt. Deborah Barasa alisema kuwa kati ya watu waliosajiliwa, karibu 7.2 milioni walitoka katika Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF), ilhali 6.2 milioni ni washiriki wapya. "Nina furaha kutambua kwamba, kufikia sasa, Wakenya 13,344,674 wamejiandikisha. Miongoni mwao ni 7,152,487 waliohama kutoka NHIF

ilhali 6,192,188 ni wana-chama wapya," akaeleza Dkt. Barasa.

Akizungumza katika mahojiano ya kipekee ofisini mwake katika jumba la Afya House, jijini Nairobi, Dkt. Barasa pia alifi-

**“Waliosajiliwa kwa SHA wat-anufaika kwa matibabu bila malipo katika vituo vya afya vya Level II na Level III na wanaweza kupata huduma nyingine za magonjwa ya dharura,” Barasa**

chua kuwa waajiri 29,598, pamoja na watoa huduma za afya 7,411, wamesajiliwa na SHA.

Alisema kuwa walengwa wa SHA wanaotafuta huduma za matibabu katika vituo vya Level II na Level III kote nchini wata-pata matibabu bila malipo yoyote.

“Waliojisajili wa SHA watafaidika na matibabu ya bure katika vituo vya Level II na Level III na kupata huduma muhimu chini ya fedha za dharura za magonjwa sugu,” akasema Waziri.

Dkt. Barasa alisema kwamba, chini ya mchanganuo wa faida za madai ya SHA, serikali imetenga kiasi cha Sh102.8



Waziri wa Afya Dkt. Deborah Barasa

ENDELEA UK 2

**13M**

Wakenya walio-kuwa wamejiandikisha kwa Mamlaka mpya ya Afya ya Jamii (SHA) kufikia Oktoba 31, 2024

**Sh8.5B**

Gharama ya Chuo cha Utalii cha Ronald Ngala eneo la Vipingo ambacho kinakaribia kukamilika baada ya kukwama kwa miaka 14

**5.7B**

Kiasi cha pesa ambacho Serikali imetumia katika ujenzi unaoendelea wa nyumba za bei nafuu katika Kaunti ya Kisumu.

**49M**

Ruzuku iliyotangazwa na Rais William Ruto kusaidia Tamasha la Utalii na Utamaduni la Turkana, Tobong'u Lore.

**Sh30B**

Gharama ya mpango ambao Mamlaka ya Rasimilali za Maji (WRA) imezindua ili kuharakisha udhibiti wa maji kwa miaka mitano ijayo.

**Sh30B**

Kiasi cha pesa ambazo hospitali zinadai kutoka kwa Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF) ambayo ilivunjwa.

**Takwimu za Wiki**

## Wakulima kufaidika kwa bei ya mahindi ya Sh3,500 serikali ikihifadhi chakula

NA **JOSEPH NG'ANG'A**, KNA

**S**erikali, kupitia Hal-mashauri ya Kitaifa ya Nafaka na Mazao (NCPB), itanza mara moja kununua magunia milioni moja ya kilo 90 za mahindi kutoka kwa wakulima kwa bei ya Sh3,500 kwa gunia kwa kila gunia la mahindi inaniwa kuwasaidia wakulima kudumisha viwango vya faida na kuwiana na bei iliyopo ya Sh2,835.

Waziri wa Kilimo na Ustawi wa Mifugo Dkt. Andrew Karanja amesema kwamba bei iliyowekwa ya Sh3,500 kwa kila gunia la mahindi inaniwa kuwasaidia wakulima kudumisha viwango vya faida na kuwiana na bei iliyopo ya Sh2,835.

"Wakati wa mvua za muda mfupi za 2022/2023, Serikali ya Kenya Kwanza ilizindua mpango wa ru-zuku ya mbolea ili kuimarisha uzalishaji wa kilimo na kuhakikisha usalama wa chakula kwa Wakenya wote kwa kupunguza gharama ya mbolea kutoka Sh6,500 hadi Sh2,500 za sasa kwa mfuko wa kilo 50," akaeleza Dkt. Karanja.

Waziri aliongeza kwamba jumla ya wakulima milioni 6.45 wamesajiliwa kwa ufanisi kwenye Mfumo wa Taarifa za Kilimo Jumuishi wa Kenya (KIAMIS), juk-



Waziri wa Kilimo na Ustawi wa Mifugo Dkt. Andrew Karanja

ENDELEA UK 2



# Wakulima kufaidi kwa bei ya Sh3,500 ya mahindi serikali ikihifadhi chakula

## ENDELEA KUTOKA UK 1

waa ambalo limeweze-sha usimamizi bora wa mpango wa ruzuku kupitia mfumo wa e-vocha.

Dkt. Karanja alieleza kwamba ruzuku ya mbolea, pamoja na hali nzuri ya hewa, imesababisha kuimarika kwa uzalishaji wa mahindi.

"Uzalishaji wa mahindi kwa msimu wa mvua ndefu wa 2024 unatarajiwa kufikia magunia milioni 75.97 ya kilo 50," akasema Dkt. Karanja.

Waziri alisisitiza kwamba, kulingana na

Ajenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya Botom-Up ili kuhakikisha gharama ya chini ya maisha, bei ya Sh3,500 pia itasaidia kudumisha bei ya sasa ya unga wa mahindi, ambayo inauzwa kwa Sh130 kwa pakiti ya kilo mbili.

"Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, kwa ushirikiano na serikali za kaunti, itatoa usaidizi wa kujenga uwezo kuhusu viwango vya ubora na mbinu za usimamizi baada ya kuvuna ili kupunguza kupotea na kuharibika kwa chakula," akasema Dkt. Karanja.



# Wakenya 13m sasa wameandikishwa kwa Mamlaka mpya ya Afya ya Jamii

## ENDELEA KUTOKA UK 1

milioni kwa ajili ya huduma za afya ya akili.

"Chini ya uchanganuzi wa manufaa ya madai, huduma kumi bora zilizotolewa ndani ya SHA katika mwezi wa kwanza zilijumuisha huduma za afya ya akili, ambazo hazikuwa zimetolewa hapo awali chini ya NHIF, ambazo ni Sh102.8 milioni," akasema.

Waziri alisema huduma zingine ni pamoja na huduma za wagonjwa wanaotibiwa na kurudi nyumbani za jumla ya Sh273.8 milioni, huduma za wagonjwa wanaolazwa Sh774.9 milioni, huduma za figo Sh244.4 milioni, pamoja na huduma za magonjwa ya damu, huduma za kina mama na watoto.

Dkt. Barasa pia alisema kuwa Wizara imeweka mikakati ya kutosha kuwezesha kushughulikiwa kwa haraka wa madai ndani ya siku 90.

"Kuanzia sasa, madai yatashughulikiwa ndani ya siku 90 ili kudumisha uendeleu na mwitikio katika utoaji wa huduma za afya," akasema.



Makao Makuu ya Mamlaka ya Afya ya Jamii (SHA) jijini Nairobi. (Picha: SHA)

Waziri aliongeza kuwa mfumo wa SHA sasa unafanya kazi kikamilifu, huku masuala ya awali ya kiufundi yakitatuliwa ipasavyo ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora.

Alisisitiza kwamba timu iliyojitolea ya taaluma mbalimbali imehamasishwa katika ngazi za mikoa na kaunti ili kusaidia na kuboresha huduma katika vituo vyote vya huduma za afya, kuhakikisha mwendelezo wa utoaji huduma chini ya SHA.

Dkt. Barasa alisisitiza kuwa usajili wa SHA, ambao uko wazi kwa Wakenya wote, unahakikisha kila mtu, bila kujali eneo au asili, anaweza kupata huduma bora za afya.

"Mfumo huu umeundwa kujumuisha watu wote, ikimaanisha kuwa vituo vya afya vya umma, vya kibinafsi na vya kidini kote nchini Kenya vinafanya kazi chini ya miongozo, viwango na huduma sawa za SHA.

Uthabiti huu unahakikisha kuwa watu waliosajiliwa wanapata huduma na manufaa sawa," akaeleza Dkt. Barasa.

Aliwataka Wakenya ambao bado hawajaiandikisha na SHA wafanye hivyo, akisema itawasaidia kupata huduma za afya za kina.

Ili kujiandikisha, watu wanatakiwa kupiga Msimbo wa USSD \*147# au kutembelea mitandao ya AfyaYangu.go.ke au SHA.go.ke.



**KENYA INSTITUTE OF MASS COMMUNICATION**  
P.O. Box 42422 - 00100 NAIROBI | Uhoho Road, Nairobi South B, off Mombasa Road  
Cell: 0708 262 895 Tel: +254 020 6997000 | Email: info@kimc.ac.ke | Website: www.kimc.ac.ke

## TENDER NOTICE

Kenya Institute of Mass Communication (KIMC) is the oldest middle level state media training Institution in Kenya established in 1961 is a State Corporation established through Legal Notice No.197 of 2011 (amended). The Institute offers training at Post graduate, Diploma and Certificate Levels in Communication and Cinematic Arts.

The Institute hereby invites bids from eligible bidders for the tender for Provision of events Management services (**Two Years frame work Contracting**).

| S/N | Tender Name                             | Reservation | Tender No.          | Closing Date                                |
|-----|-----------------------------------------|-------------|---------------------|---------------------------------------------|
| 1   | Provision of events management services | Open Tender | KIMC/S/16/2024-2026 | 11 <sup>th</sup> November, 2024 at 10.30Am. |

- Bidders are advised to download the long the Detailed Tender document from the Institutes website: [www.kimc.ac.ke](http://www.kimc.ac.ke) and PPIP Portal; [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke)
- Bidders who download the tender document must forward their particulars immediately to: [procurement@kimc.ac.ke](mailto:procurement@kimc.ac.ke) to facilitate any further clarification or addendum if any.
- Bidders may obtain further information from the Procurement Unit of KIMC at the address below during working hours from 9.00 to 16.00 Hours local time Monday to Friday.

**The Director,**  
**Kenya Institute of Mass Communication**  
**Located on Uhoho Road Nairobi south B,**  
**off Mombasa Road.**  
**P.O.Box 42422-00100 Nairobi**  
**Tel.020 6997000/0708262895**





**JOMO KENYATTA UNIVERSITY OF AGRICULTURE AND TECHNOLOGY**  
**P.O. BOX 62000 - 00200, CITY SQUARE, NAIROBI, KENYA.**  
**TEL: (067) 5870001-5, TENDER SECTION TEL No: (067) 5870000.**  
**Email: [tenders@jkuat.ac.ke](mailto:tenders@jkuat.ac.ke), Website: [www.jkuat.ac.ke](http://www.jkuat.ac.ke)**

## TENDER NOTICE

Jomo Kenyatta University of Agriculture & Technology intends to lease the two parcels of land measuring approximately 2.013 acres situated at Jipe Close – Lavington Estate, Nairobi City County. The University now invites sealed tenders from eligible candidates to lease the said property. The lease period is for ten (10) years, renewable under a lease agreement.

Interested Bidders are invited to apply for Tender listed below.

| S/No. | Tender Reference No.    | Description of Tender                                                  | Eligibility |
|-------|-------------------------|------------------------------------------------------------------------|-------------|
| 1     | REF: JKUAT/69/2023-2024 | Lease of property L.R. No. 5/38 & L.R. No. 5/39 JKUAT Westlands Campus | Open        |

**A tenderer must tender for the two parcels of land as tabulated above.**

Interested tenderers may inspect the said property to be leased during office hours **Monday to Friday 9.00 am to 4.00 pm.**

Interested and eligible candidates may inspect and obtain Tender Document from the University's Department of Procurement at JKUAT – Main Campus or download documents from our website: [www.jkuat.ac.ke](http://www.jkuat.ac.ke) free of charge from PPIP portal: Public Procurement Information Portal [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke).

The Tenderers should stamp and serialize all pages and **SHOULD NOT** alter the Bid Document.

Sealed Tenders must be accompanied by duly completed forms as specified in the Bid Documents with Original and a copy in the same envelop and addressed to:

**Vice Chancellor,**  
**Jomo Kenyatta University of Agriculture and Technology,**  
**P.O. Box 62000 - 00200, Nairobi.**

and placed in the Tender Box at the **Department of Procurement JKUAT Main Campus**. The documents should be in plain sealed envelopes indicating the Tender Number, without identifying the sender so as to reach the University not later than **Tuesday 19th November, 2024 at 11:30 a.m.** Bids will be opened immediately thereafter at **Procurement Department, JKUAT Main Campus** in the presence of bidders/their representatives who wish to attend.



**JKUAT is ISO 9001:2015 and ISO 14001:2015 Certified**  
*Setting Trends in Higher Education, Research, Innovation and Entrepreneurship*





# Serikali kulipa deni la NHIF la Sh30 bilioni kufuatia kuanza kwa Hazina ya Afya ya Jamii

NA JANE NGUGI, KNA

Serikali italipa Sh30 bilioni ambazo hospitali zinadai Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF) kama sehemu ya mabadiliko yanayoendelea ya Hazina ya Bima ya Afya ya Jamii (SHIF).

Katibu Mkuu wa Huduma za Matibabu Bw. Harry Kimtai alisema kuwa Sh4.5 bilioni tayari zimetolewa kwa vituo vya afya, na Sh4.5 bilioni za ziada zitatolewa baadaye wiki hii.

Bw. Kimtai alitangaza kuwa serikali imejitolea kulipa vituo vya huduma za afya Sh9 bilioni kufikia mwisho wa Novemba.

Aliongeza kuwa Serikali imeagiza Makamishna wa Kaunti na Wajumbe wa Kamati Kuu za Kaunti (CECM) wanaohusika na huduma za afya wahakikishe wanachama wanaolipwa kikamilifu wa Hazina ya Bima ya Afya ya Jamii (SHIF) hawanyimwi huduma.

Akizungumza mjini Nakuru baada ya kukutana na Makamishna wa Kaunti

na CECM kutoka kaunti 14 za eneo la Bonde la Ufa, Katibu Mkuu aliwashauri Wakenya waliosajiliwa na SHIF waweke majina ya watu wao kwenye tovuti ya hazina hiyo ili kuhakikisha wanaweza kupata manufaa wakati wowote inapohitajika.

Bw Kimtai alisema umuzi wa kulipa Sh30 bilioni ni hatua muhimu ya kudumisha uaminifu na ushirikiano wa vituo vya afya chini ya SHIF. Aliahidi kuwa malipo yaliyobakia yatafanywa hatua kwa hatua, kwa kutegemea upatikanaji wa fedha.

Hospitali na watoaji huduma wengine wa afya walisita kuhamia SHA kutokana na matatizo ya kifedha yaliyosababishwa na madai ambayo hayajalipwa.

Katibu Mkuu alisema kamati ya uongozi ya kitaifa ambayo inawaleta wadau wote katika sekta ya afya imeundwa ili kusaidia kulainisha mabadiliko kutoka NHIF hadi SHIF.

“Tunakubali kumekuwa na hitilafu wakati wa ku-

hamia kwa SHIF, lakini tunataka kuwahakikishia Wakenya kwamba tunatatua changamoto hizo na hivi karibuni shughuli katika hazina hiyo mpya zitaendeshwa bila matatizo.

“Serikali imejitolea kuhakikisha kila Mkenya anapata huduma bora za afya na za bei nafuu,” akasema Katibu Mkuu.

Kulingana na wasimamizi wa baadhi ya hospitali, kiasi kilichosalia kimezua changamoto za kiutendaji, huku baadhi ya vituo vikilazimika kuchelewesha huduma au kutafuta njia mbadala za kuendelea kufanya kazi.

Kama sehemu ya mabadiliko hayo, Bw Kimtai aliwahakikishia washikadau kwamba serikali itashughulikia wajibu huu uliosalia wa kifedha.

Alisema wasiwasi wa hospitali nyingi kuhusu mpito na madeni ni halali na utashughulikiwa kwa wakati unaofaa.

“Tutachukua mali na madeni ya NHIF. Deni letu linakadiriwa kuwa karibu Sh30 bilioni,” akasema.

Wizara ya Afya, alisema,



Katibu Mkuu wa Huduma za Matibabu, Harry Kimtai, katika hafla ya awali. Ametoa hakikisho kwamba serikali italipa Sh30 bilioni ambazo hospitali zinadai Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF) kama sehemu ya mabadiliko yanayoendelea ya Hazina ya Bima ya Afya ya Jamii (SHIF).

imeunda kamati ya mpito ambayo imekuwa iki-chunguza mali na madeni ya NHIF.

“Pia tumeunda kamati ambayo itasimamia malipo ya madai na utoaji wa fedha. Hatutapendelea hospitali yoyote kuhusi-ana na malipo,” akasema.

“Kiasi chochote tulichonacho katika wizara tutatumia asilimia moja tu na kutangaza kuwa kati ya fedha tulizonazo tutalipa hospitali kwa kiwango

cha juu na kumaliza madeni hayo ili kuwahakikishia kuwa hakutakuwa na madeni yanayoendelea kwa kipindi cha mpito,” akaongeza Bw Kimtai.

Katibu Mkuu alisema katika kipindi cha mpito, malipo ya madai hayatacheleweshwa kwa kuwa mfumo wa sasa unaweza kufuatilia madai yanap-olingia, mfumo huo hadi Jumanne wiki iliyopita ukiwa na Sh100 milioni zitakazolipwa hospitalini.

“Tumetoa agizo kwa SHA (Mamlaka ya Afya ya Jamii) kwamba wana-takiwa kulipa madai hayo ndani ya siku 90 baada ya kuwasilishwa. Hii italeta kujiamini na kuridhika kwa kila mtu. Tunataka kuwa na akili timamu kuhakikisha kwamba wana-aoewekeza katika biashara wana hakika ya mapato yao ili waweze kukua,” akasema.

Katibu Mkuu alitetea Hazina ya Bima ya Afya ya Jamii (SHIF) ambayo imesababisha mabadiliko makubwa katika sekta ya afya, akisema upungufu unaojitokeza unatokana na matatizo ya awali.

Alisisitiza kuwa hazina mpya ya Bima ya Afya ya Jamii (SHIF), licha ya kuanzishwa kwake kwa kuyumba, iko tayari kubadilisha upatikanaji wa huduma za afya.



## BOMET UNIVERSITY COLLEGE

(A Constituent College of Moi University)

### TENDER NOTICE

Bomet University College invites interested, eligible and capable firms for provision of Goods, Works and Services for the Financial Year 2024/2025

| S/N | Tender No.                           | Item Description                                                                                                                                                | Eligibility | Closing Date                                |
|-----|--------------------------------------|-----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------|---------------------------------------------|
| 1.  | BUC/OT/ICT/08/2024-2025              | Supply and Delivery of the following: <ul style="list-style-type: none"><li>Document Management System,</li><li>Severs and</li><li>Biometric Terminal</li></ul> | Open to All | 15 <sup>th</sup> November, 2024 at 10:00 am |
| 2.  | BUC/OT/FRWC/09/2024-2025 & 2024-2026 | Provision of Motor Vehicle Maintenances Services                                                                                                                | Open to All |                                             |
| 3.  | BUC/OT/010/25/2024-2025              | Supply and Delivery of Library Books                                                                                                                            | Open to All |                                             |
| 4.  | BUC/PQ/2024-2026 FY                  | Registration of Suppliers for Supply and Delivery of Goods, Works and Services for Financial Year 2024-2025/2025-2026                                           | Open to All |                                             |

Interested eligible Bidders who wish to apply may obtain Tender Documents with detailed requirements and conditions, from the Procurement Office at a non-refundable fee of **Kshs. 1,000** per set, between 8.00 am to 5.00 pm on working days, or download from the University Website: [www.buc.ac.ke](http://www.buc.ac.ke) or Public Procurement Information Portal (PIIP) tender portal [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke) to access further details in regard to the tenders. Bidders are required to complete and submit the Tender Documents in a plain sealed envelope, clearly marked "Tender No" addressed to **Principal, Bomet University College, P.O Box 701-20400, Bomet**, and deposit in the Tender Box at the Reception in the Green Tuition Block at Bomet University College, on or before: **Friday, 15<sup>th</sup> November, 2024 at 10:00 am**. Tenders will be opened immediately thereafter in the presence of Bidders or their Representatives who choose to attend.

Bidders are advised to regularly visit Bomet University College website to obtain any additional information/ Addendum on the Tenders which will form part of the Tender Document.

Any Canvassing will lead to automatic disqualification. **Late Tenders will not be accepted.**  
Youth, Women and Persons with disability are encouraged to apply.

**PRINCIPAL  
BOMET UNIVERSITY COLLEGE  
P.O BOX 701 – 20400  
BOMET**

**GREEN ECONOMY FOR SUSTAINABILITY**



## KENYA UTALII COLLEGE

Gateway to International Careers in Hospitality & Tourism

### NOTICE OF THE 48TH GRADUATION CEREMONY

This is to notify **ALL** graduands that Kenya Utalii College will hold its **48<sup>th</sup> Graduation Ceremony** on **Thursday, 5<sup>th</sup> December, 2024 at 10:00 am** at the College Library grounds, along Thika Super Highway. The proceedings of this event will also be streamed live on Kenya Utalii College Social Media platforms (**YouTube and Facebook**). The links for the event will be provided at least two days to the event.

#### ACADEMIC ATTIRE

**ALL** graduands will be required to be in full academic attire during the ceremony. Food Production will wear their professional Chefs Uniform. The attire will be issued at the Laundry Department from **Tuesday 3<sup>rd</sup> to Wednesday, 4<sup>th</sup> December, 2024** during working hours (8:00 am to 5:00 pm).

#### RETURN OF GOWNS

**ALL** graduands are required to return the gowns latest by **4.00 pm, Friday, 13<sup>th</sup> December, 2024** failure to which a fine of **Kes 200/- per day** shall be levied for any attire returned after the said deadline.

#### REHEARSAL

It is **MANDATORY** that **ALL** graduands attend the rehearsal at the Library Grounds on **Wednesday, 4<sup>th</sup> December, 2024 at 9:00 am**. Graduands should be seated by 8:30 am.

#### GRADUATION FEES

The Graduation fee is **Kes 3,500/-**.  
All graduands are required to pay the non-refundable graduation fee into the  
a) College Fees **Account No. 01129070937100, Co-operative Bank, Stima Plaza Branch** Or via  
b) **Mpesa Paybill number 222222, Account number: KUCC2-Student Number**  
(Note: Every transaction attracts an additional Kes 50 for E-Citizen)

by **Friday, 29<sup>th</sup> November, 2024**. Graduands will be required to produce bank slips to the College cashier for issuance of receipts by the aforementioned date. **Cash payments will not be accepted.**

**Note:** Only those students who have fully paid the College fees, graduation fees, and cleared with the Examinations Office will be eligible for graduation. For any enquiries on examinations please contact the Examinations Office through email: [examinations@utalii.ac.ke](mailto:examinations@utalii.ac.ke).

For more information on the graduation ceremony and courses offered, please log on to our College website: [www.utalii.ac.ke](http://www.utalii.ac.ke)



# Mpango wa Sh30 bilioni wazinduliwa kuboresha huduma za maji Kenya

NA JOAN OGOLLA NA MANU MUMBA, KNA

Mamlaka ya Rasilimali za Maji (WRA) imezindua mpango wa Sh30 bilioni ili kuharakisha udhibiti wa maji katika azma ya kuboresha upatikanaji wa bidhaa hiyo adimu katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati wa mamlaka hiyo jijini Nairobi, Waziri wa Maji, Usafi wa Mazingira na Unyunyizaji Mhandisi Eric Mugaa alisema kuwa mpango huo unalenga kudhibiti usimamizi na matumizi ya rasilimali za maji kwa ustawi.

"Mpango huu unawiana na Ruwaza ya Kenya ya 2030 na Ajenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya Bottom-Up, kwa sababu unalenga kushughulikia masuala kama vile kufuata sheria za rasilimali za maji, ushirikiano wa mabadiliko ya hali ya hewa, ush-

irikiano wa washikadau, na kukusanya rasilimali," akaema Mhandisi Mugaa.

Alisema malengo ya mpango huo ni kufanya kazi na kudumisha ukusanyaji wa taarifa za rasilimali za maji, kuimarisha mipango na ugawaji wa maji, kuongeza uwezo wa kitaasisi wa WRA, na kuboresha uhifadhi wa maeneo ya vyanzo vya maji.

Waziri alisema mpango huo utaelekeza WRA kufikia malengo yake katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alifichua kwamba mpango huo unahusisha mambo muhimu kama vile kuweka huduma kidijitali na kukuza data ya wakati halisi ili kufuatilia na kuchambua maeneo yanayokumbwa na mafuriko.

Waziri alitoa wito wa ushirikiano kutoka kwa washirika wa kimaendeleo, sio tu kuunga mkono WRA, lakini pia wizara nzima katika masuala ya

maendeleo na udhibiti wa maji.

"Maji yanapotua-cha, yanaelekezwa kwa mashirika mengine ambayo yanashughulikia mabwawa na utoaji wa huduma hadi ngazi ya kaunti na kwa hivyo WRA ikishindwa katika majukumu yake, mambo mengine yote yatashindwa," akasisitiza.

Katika hotuba yake, Katibu Mkuu wa Idara ya Maji na Unyunyizaji Julius Korir alisema WRA inafanya kazi ndani ya mfumo uliotumika katika Sheria ya Maji ya 2016 ambayo inatimiza jukumu la kuweka kipaumbele maendeleo endelevu ya maji ya ardhi.

"WRA imefikia hatua muhimu katika kuimarisha ustahimilivu wa mabadiliko ya hali ya hewa na usalama wa maji," akatangaza.

Korir alifichua kuwa idara ya serikali inachangia maendeleo ya kitaifa kwa kusaidia



Waziri wa Maji, Usafi wa Mazingira na Unyunyizaji, Mhandisi Eric Mugaa. Picha: Manu Mumba/KNA.

usimamizi jumuishi wa rasilimali za maji ili kuimarisha upatikanaji na ufikiaji wa maji.

Alibainisha kuwa maji yanayopatikana kwa mwaka kwa kila mtu ni mita za ujazo 106 ikilinganishwa na mita za ujazo 600 zinazohitajika kwa mwaka.

"Ni juu yetu kuhakikisha kuwa tuna hifadhi ya maji ya kutosha ili kuweza

kukidhi mahitaji ya wateja wetu," akasema.

Mpango mkakati wa WRA ulitengenezwa kama mwendelezo wa mpango wa 2018 hadi 2022. Mpango huo unakuja wakati ambapo hali mbaya ya mazingira yakiwemo mabadiliko ya hali ya hewa na ongezeko la joto yamesababisha kushuka kwa hifadhi ya maji chini ya ardhi.

Ni wakati ambao pia Ajenda ya Mabadiliko ya Kiuchumi ya Bottom-Up imezinduliwa kwa lengo la kuimarisha sekta ya viwanda na kilimo ili kuendeleza maendeleo ya kiuchumi nchini Kenya.

Ajenda hiyo inategemea maji kama hitaji muhimu, kwa hivyo ni muhimu kuimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali za maji.



**MINISTRY OF WATER, SANITATION AND IRRIGATION**  
**STATE DEPARTMENT FOR WATER AND SANITATION**

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST FOR**  
**CONSULTANCY SERVICES FOR ENVIRONMENT AND SOCIAL SAFEGUARDS (E&S) CAPACITY NEEDS ASSESSMENT AND DEVELOPMENT OF A CAPACITY ENHANCEMENT PLAN FOR THE KENYA WATER SECTOR**

**CONTRACT NO.: KE-MOWI-441576-CS-CQS**

**ADDENDUM NO.1**  
**EXTENSION OF SUBMISSION DEADLINE**

1. The Invitation to Tenders (ITT) Submission Deadline is hereby extended from 5<sup>th</sup> November, 2024 to **12<sup>th</sup> November, 2024 at 10.00 a.m.**

2. All other terms and conditions remain the same.

**HEAD OF SUPPLY CHAIN MANAGEMENT SERVICES**  
**For: PRINCIPAL SECRETARY**  
**STATE DEPARTMENT FOR WATER AND SANITATION**

**Ministry of Water, Sanitation and Irrigation**  
**Maji House, Ngong Road**  
**2<sup>nd</sup> Floor Room No. 233**  
**P.O. Box 49720-00100, Nairobi.**  
**Tel: +254 20 2716103 Ext. 42112**  
**Email: [hoagw4rp@water.go.ke](mailto:hoagw4rp@water.go.ke)/[hoagw4rp@gmail.com](mailto:hoagw4rp@gmail.com)**  
**Website: [www.water.go.ke](http://www.water.go.ke)**





**KIBABII UNIVERSITY**  
**EXTERNAL ADVERTISEMENT FOR TEACHING AND ADMINISTRATIVE VACANCIES**

Pursuant to Part V Section 35 of the Universities Act 2012, Part IV Section 23 of the Kibabii University Charter, 2015 and Kibabii University Statutes 2023, the University invites applications from suitably qualified applicants for the following vacant positions:

| TEACHING POSITIONS       |                                                                |       |                  |              |
|--------------------------|----------------------------------------------------------------|-------|------------------|--------------|
| S/No.                    | Designation                                                    | Grade | Advert No.       | No. of Posts |
| 1.                       | Lecturer/Research Fellow (Strategic Management)                | AC 12 | KIBU/ACA/13/2024 | 1            |
| 2.                       | Tutorial/Junior Research Fellow (Religion)                     | AC 11 | KIBU/ACA/14/2024 | 1            |
| 3.                       | Tutorial/Junior Research Fellow (Criminology)                  | AC 11 | KIBU/ACA/16/2024 | 1            |
| 4.                       | Tutorial/Junior Research Fellow (Midwifery) (Re-advertisement) | AC 11 | KIBU/ACA/17/2024 | 1            |
| Sub-total                |                                                                |       |                  | 4            |
| ADMINISTRATIVE POSITIONS |                                                                |       |                  |              |
| S/No.                    | Designation                                                    | Grade | Advert No.       | No. of Posts |
| 1.                       | Chief Supply Chain Management Officer - (Re-advertisement)     | AD 15 | KIBU/ADM/10/2024 | 1            |
| 2.                       | Dean of Students - (Re-advertisement)                          | AD 15 | KIBU/ADM/11/2024 | 1            |
| 3.                       | Senior Accountant                                              | AD 13 | KIBU/ADM/12/2024 | 1            |
| 4.                       | Assistant Games and Sports Officer III - (Re-advertisement)    | AD 5  | KIBU/ADM/13/2024 | 1            |
| 5.                       | Driver I- (Re advertisement)                                   | AD 4  | KIBU/ADM/14/2024 | 2            |
| Sub-total                |                                                                |       |                  | 6            |
| Grand Total              |                                                                |       |                  | 10           |

Applications must be submitted on or before **5 pm EAT Tuesday 19<sup>th</sup> November, 2024.**

**Note:** For more details on this advertisement, please visit the University website and click on the following link: <https://kibu.ac.ke/jobs-vacancies/>.



**Kibabii university ISO 9001:2015 Certified**  
**Knowledge for Development**



# Ujenzi wa Sh8.5b wa Ronald Ngala Utalii College wakaribia kumalizika

NA SADIK HASSAN, KNA

Baada ya kukwama kwa miaka 14, ujenzi wa Chuo cha Utalii cha Ronald Ngala cha Sh8.5 bilioni eneo la Vipingo hatimaye umeanza tena. Mradi huo ulikuwa umekwama kwa miaka mingi kutokana na madai ya ufiisadi.

Waziri wa Utalii na Wanyamapori, Rebecca Miano, hivi majuzi alitembelea kituo hicho cha kuvutia, ambacho kinachukua ekari 59 karibu na Bahari ya Hindi. Alisema taasisi hiyo iko tayari kuwa kitovu cha ubora kwa sekta ya utalii kulingana na Ruwaza ya 2030.

Chuo hicho kinatarajiwa kuimarisha sekta ya Uchumi wa Uchumi Samawati na Utalii wa Baharini kwa kutoa mafunzo maalumu, na hivyo kuimarisha maendeleo ya



Waziri wa Utalii Rebecca Miano akionyesha mfano wa mradi huo wakati wa ziara yake katika Ronald Ngala Utalii College, eneo la Vipingo.

ujuzi na kujenga uwezo.

"Kazi nyingi zimefanaywa, na mradi sasa umekamilika kwa karibu asilimia 83," akasema Waziri Miano, akiandamana na wajumbe wa bodi kutoka Hazina ya Utalii. Waziri pia alifanya mkutano na bodi kujadili mpango wa uendeshaji na ratiba ya ufunguzi wa

chuo hicho. "Tunatumai kitakuwa tayari kufikia mwisho wa robo ya kwanza ya mwaka ujao," akasema.

Waziri alipongeza Hazina ya Udhhamini wa Utalii kwa kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha mradi huo unaendelea kama ilivyopangwa.



## INVITATION TO TENDER

Kenya Power invites tenders from interested bidders for provision of the following:-

| NO. | TENDER NO.                 | ITEM DESCRIPTION                                                                                                        | TENDER COMMENCEMENT DATE | TENDER CLOSING DATE               |
|-----|----------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|--------------------------|-----------------------------------|
| 1.  | KP9/9A/OT/WK/TPT/001/24-25 | Three (3) Year Contract for Supply of Fleet Repair & Maintenance Service from Third Party Garages for West Kenya Region | Tuesday 05.11.2024       | Tuesday 26.11.2024 at 10.00 a.m.  |
| NO. | TENDER NO.                 | REGISTRATION NO.                                                                                                        | TENDER COMMENCEMENT DATE | TENDER CLOSING DATE               |
| 2.  | 3800000430                 | Registration of Suppliers and Contractors for Generator Spare Parts, Works and Services for Off Grid Power Stations     | Thursday 07.11.2024      | Thursday 21.11.2024 at 10.00 a.m. |

Tender documents detailing the requirements of the above tender may be obtained from the Kenya Power website ([www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke)) from the dates shown above.

GENERAL MANAGER  
SUPPLY CHAIN & LOGISTICS

[www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke)

DIAL \*977# | Access Kenya Power services fast and easy

[www.kplc.co.ke](http://www.kplc.co.ke) | Customer Care 020 200 0000 | Kenya Power | 020 200 0000 | 0708-070 700, 0752-070 170



## BOMET UNIVERSITY COLLEGE

(A Constituent College of Moi University)

### VACANT POSITIONS FOR REPLACEMENT

Bomet University College (BUC) is a Constituent College of Moi University established through the Legal Notice No. 145 of 27th July 2017. BUC is located in Bomet County. The University College invites applications from suitably qualified candidates for the following Positions that have fallen vacant:

#### ACADEMIC POSITIONS

| S/N | POSITION        | SPECIALIZATION                   | SCALE  | NO. | JOB REFERENCE     |
|-----|-----------------|----------------------------------|--------|-----|-------------------|
| 1   | Senior Lecturer | Computer Science                 | BUC 13 | 1   | BUC/ACD/1/11/2024 |
| 2   | Lecturer        | Physics (Electronics)            | BUC 12 | 1   | BUC/ACD/2/11/2024 |
| 3   | Lecturer        | Communication / Public Relations | BUC 12 | 2   | BUC/ACD/3/11/2024 |
| 4   | Lecturer        | History                          | BUC 12 | 1   | BUC/ACD/4/11/2024 |

#### ADMINISTRATIVE POSITIONS

| S/N | POSITION                        | SCALE | NO. | JOB REFERENCE       |
|-----|---------------------------------|-------|-----|---------------------|
| 1   | Senior Procurement Officer      | BUC13 | 1   | BUC/ADM/1/11/2024   |
| 2   | Senior Accountant               | BUC13 | 1   | BUC/ADM/2/11/2024   |
| 3.  | Quantity Surveyor               | BUC10 | 1   | BUC/ADM/3/11/2024   |
| 4   | Senior Administrative Assistant | BUC10 | 1   | BUC/ADM/4/11/2024   |
| 5   | Legal Assistant II              | BUC 8 | 1   | BUC/ADM/5/11/2024   |
| 6   | Secretary                       | BUC 7 | 1   | BUC/ADM/ 6/11/2024  |
| 7   | Assistant Farm Manager          | BUC 7 | 1   | BUC/ADM/ 7/11/2024  |
| 8   | Clerical Officer                | BUC 5 | 2   | BUC/ADM/ 8/11/2024  |
| 9   | Security Officer                | BUC 5 | 1   | BUC/ADM/ 9/11/2024  |
| 10  | Security Supervisor             | BUC 4 | 1   | BUC/ADM/ 10/11/2024 |

Qualifications for the advertised Academic Positions are based on Commission for University Education (CUE) Harmonized Criteria for Appointment and Promotion of Academic Staff. Please visit Commission for University Education (CUE) website for more information.

**Terms of Service:** All the Positions listed above are on Permanent and Pensionable terms, subject to successful completion of Probation period of six (6) months.

**GENERAL REQUIREMENTS FOR THE POSITIONS.** Only shortlisted applicants will be conducted and will be expected to satisfy requirements of the Chapter Six of the Constitution of Kenya (2010) when successful in the Recruitment process.

Interested applicants should visit the Bomet University College website <https://www.buc.ac.ke> for detailed Job Specifications, Remuneration and other job requirements. The Reference Number of the Position applied for should be clearly indicated in the Applications letter addressed to: **The Principal, Bomet University College, P.O Box 701-20400, BOMET.** A signed Application letter with the required testimonials should be emailed to: [recruitment1@buc.ac.ke](mailto:recruitment1@buc.ac.ke) on or before **Monday 25<sup>th</sup> November 2024 at 5.00 pm.**

Bomet University College is an Equal Opportunity Employer and does not charge any fee for recruitment.

Persons having difficulties in performing activities of daily life and marginalized groups are encouraged to apply.

GREEN ECONOMY FOR SUSTAINABILITY



## MINISTRY OF INVESTMENTS, TRADE AND INDUSTRY

### State Department for Industry

## PUBLIC NOTICE

### THE DRAFT NATIONAL COTTON, TEXTILE AND APPAREL POLICY

The Ministry of Investments, Trade and Industry in collaboration with relevant Ministries, Departments and Agencies has developed a draft National Cotton, Textile and Apparel Policy, 2024 to guide the development of the cotton value chain in Kenya. The policy also aims to revitalize and enhance the competitiveness and sustainability of the Cotton, Textiles and Apparel sector in Kenya and within the region.

Pursuant to Article 10(2) (a) of the Constitution of Kenya, that provides for National Values and Principles of Governance including participation of the people, the Ministry through this Notice, hereby invites interested members of the public and stakeholders to give their comments on the draft National Cotton, Textile and Apparel Policy during the public participation forums which shall be held from 9.00 a.m-12.00 noon at the following venues and dates;

| DATE                                    | COUNTIES                               | VENUE                                                                                 |
|-----------------------------------------|----------------------------------------|---------------------------------------------------------------------------------------|
| Monday 2 <sup>nd</sup> December 2024    | Laikipia, Samburu, Isiolo and Marsabit | Isiolo Catholic Pastoral Center-Isiolo                                                |
|                                         | Bomet, Nyamira, Kisii and Narok        | Kisii Agricultural Training Center Hall - Kisii                                       |
|                                         | Garissa, Wajir and Mandera             | Government Guest House – Garissa                                                      |
| Tuesday 3 <sup>rd</sup> December 2024   | Tharaka Nithi, Meru and Embu           | Kamundi Hall - Meru                                                                   |
|                                         | Tana River, Kilifi and Lamu            | Takaye Social Hall – Malindi                                                          |
|                                         | Homa Bay, Kisumu, Siaya and Migori     | Mama Grace Onyango Cultural and Social Center(Formerly Kisumu Social Center) - Kisumu |
| Wednesday 4 <sup>th</sup> December 2024 | Nyeri, Nyandarua, Kirinyaga, Murang'a  | Nyeri Cultural Center - Nyeri                                                         |
|                                         | Kwale and Mombasa                      | Tononoka Social Hall - Mombasa                                                        |
|                                         | Busia, Bungoma, Vihiga and Kakamega    | Kenya Red Cross Society Hall, Kanduyi-Bungoma                                         |
| Thursday 5 <sup>th</sup> December 2024  | Nakuru, Kericho and Baringo            | Kenya National Library Services – Nakuru                                              |
|                                         | Taita Taveta                           | Dan Mwanzo Hall – Voi                                                                 |
|                                         | Trans-Nzoia and West Pokot             | Kitale Social Hall – Kitale                                                           |
| Friday 6 <sup>th</sup> December 2024    | Machakos, Kitui and Makueni            | Wote Social Hall – Wote                                                               |
|                                         | Turkana                                | Lodwar Vocational Training Centre – Lodwar                                            |
|                                         | Uasin Gishu, Nandi and Elgeyo Marakwet | County Multi-purpose Hall – Eldoret                                                   |
| Tuesday 10 <sup>th</sup> December 2024  | Nairobi, Kajiado and Kiambu            | NITA Nairobi Headquarters Theatre Room (Commercial street, Industrial Area) – Nairobi |

Members of the Public and Stakeholders may also send their comments and feedback through written submissions using the **"Draft National Cotton, Textile and Apparel Policy, 2024 Memorandum Submission Template"** available at [www.industrialization.go.ke/downloads](http://www.industrialization.go.ke/downloads) to the following email address [cta@industrialization.go.ke](mailto:cta@industrialization.go.ke) or through **P.O BOX 30418-00100** on or before **Friday 13<sup>th</sup> December, 2024.** The Draft National Cotton, Textile and Apparel Policy may be downloaded from website [www.industrialization.go.ke/downloads](http://www.industrialization.go.ke/downloads).

# Hazina ya Biashara ya Vijana yatoa Sh300 milioni kusaidia wanaotafuta kazi nje ya nchi

NA RIPOTA WA MYGOV

Hazina ya Maendeleo ya Biashara ya Vijana (YEDF) itatoa angalau Sh300 milioni kusaidia vijana wanaotafuta nafasi za ajira nje ya nchi katika mwaka wa kifedha wa 2024/2025. Hazina hiyo inasema kuwa mpango huo unaambatana na juhudi za serikali za kutafuta Wakenya kazi ng'ambo.

"Kupitia mpango wetu wa uhamiaji, tunaondoa vikwazo vya kifedha ili kuwezesha vijana wanaostahili kupata nafasi za kazi za kimataifa ambazo hapo awali hazikufikiwa," akasema Bw. Josiah Moriasi, Afisa Mkuu Mtendaji wa Hazina hiyo.

Kulingana na Bw. Moriasi, mpango huo tayari umefikia ufanisi mkubwa, kwa kutoa Sh46.4 milioni katika miezi miwili tu kusaaidia vijana 353 kupata kazi nje ya nchi.

Moriasi aliongeza kuwa hazina hiyo inatoa mikopo isiyo na riba hadi Sh300,000 kwa vijana binafsi, na ada ya usimamizi ya asilimia nane pekee na muda wa kurudisha wa miezi sita.

"Mikopo hii inashughulikia gharama muhimu, ikiwemo nauli ya ndege, ukaguzi wa kimatibabu, na ada za utayarishaji wa vyeti vya kusafiria," akasema Bw Moriasi.



Afisa Mkuu Mtendaji wa Hazina ya Biashara ya Bw. Josiah Moriasi.

Hazina ya YEDF hutoa mikopo iliyoidhinishwa ya hadi Sh5 milioni kwa mawakala wa uajiri walioidhinishwa ambao wanataka kufanya kazi kama wasuluhishi, ikitoa muda wa ulipaji wa miezi kumi na miwili na ada ya nafuu ya asilimia mbili.

Moriasi aliongeza kuwa mpango mkuu chini ya ajenda ya kimataifa ya ajira ya YEDF ni 'Mkulima Majuu', unaunganisha wafanyakazi wa mashambani wenye ujuzi kutoka taasisi za Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) na Huduma ya Vijana kwa Taifa (NYS) na fursa za ajira katika kilimo nchini Uingereza.

Moriasi alisema mpango huo unatekelezwa kwa ushirikiano na Idara ya Serikali ya Masuala ya Ki-Geni, TVETA, na HOPS Labor Solutions (Uingereza).

Bw Moriasi aliongeza kwamba mpango wa YESA unatoa msaada wa kina kwa walengwa, yakiwemo mafunzo ya kabla ya kuondoka ili kuwaandaa kwa mazingira ya kazi nje ya nchi.

Alisema hazina hiyo imeunda ushirikiano na wadau wakuu ndani na nje ya nchi, na hivyo ku-sababisha mfumo wa kusaaidia vijana katika safari yao ya kimataifa ya ajira.

"Mpango huu utasaidia kupunguza ukosefu wa ajira nyumbani na kukuza uchumi wa nchi kupitia uhamishaji wa fedha na ujuzi," akaeleza Bw. Moriasi.

"Unaambatana na lengo kuu la serikali la kupanua fursa za ajira kwa vijana na kuwawezesha kuchangia uchumi kupitia uzoefu wa kazi wa kimataifa," akasema.



KENYA REVENUE AUTHORITY  
Tulipe Ushuru, Tujitegemee!

## Public Notice

### Declaration of Mobile Devices Incorporating IMEI Numbers at Importation

Kenya Revenue Authority (KRA) is mandated to collect revenue on behalf of the Government of Kenya. Among the tax laws and regulations it administers, KRA also administers the East African Community Customs Management Act (EACCMA, 2004).

Pursuant to Part B of the Second Schedule to the East African Community Customs Management Act (EACCMA, 2004), on restricted imports, mobile devices require regulatory permits from the Communications Authority of Kenya (CA).

Following the Communication Authority of Kenya's (CA) public notice on enhancing the integrity and tax compliance of mobile devices, Kenya Revenue Authority (KRA) hereby notifies all importers of Mobile devices and travelers of the following Customs requirements to implement the CA's requirements:

- Requirements for Importers:** All Importers of Mobile Devices will be required to submit detailed import entries for all mobile devices with accurate quantities, proper model descriptions/specifications, and their respective IMEI numbers in the Customs system.
- Requirements for Passengers:** Passengers entering the territory of Kenya will declare the details and the respective IMEI numbers for their mobile devices intended for use, during the stay in the country at the Port of entry on the F88 passenger declaration form.
- Device Assemblers/Manufacturers:** Must register on the Customs portal and submit a report of all devices assembled for the local market and their respective IMEI numbers.

One must also obtain necessary regulatory clearances and permits from the Communications Authority of Kenya (CA).

The Public is therefore notified of this requirement, which will be implemented **effective 1<sup>st</sup> January, 2025**. Specific guidelines on the system process and how to capture the devices and IMEI numbers for different users will be shared in due course.

For more information kindly email: [callcentre@kra.go.ke](mailto:callcentre@kra.go.ke), the Contact Centre on 020 4999 999 or 0711 099 999, or visit any KRA office near you.

Commissioner Customs and Border Control  
Thank you for paying your taxes!

[www.kra.go.ke](http://www.kra.go.ke)

Disclaimer: KRA notifies taxpayers that it will not accept responsibility for payments not received, credited and validated in the relevant KRA accounts. **Corruption Reporting:** +254 (0726) 984 668. Email: [corruptionreporting@kra.go.ke](mailto:corruptionreporting@kra.go.ke). **Short Messaging Services (SMS):** Dial (\*572#) or Text to 22572. Contact Centre: +254 (020) 4 999 999, +254 (0711) 099 999, Email: [callcentre@kra.go.ke](mailto:callcentre@kra.go.ke). **Complaints & Information Centre Hotlines:** +254 709 017 700 / 800 Email: [cic@kra.go.ke](mailto:cic@kra.go.ke)



KENYA REVENUE AUTHORITY  
Tulipe Ushuru, Tujitegemee!

## Public Notice

### Draft Statutory Instruments

In compliance with the Statutory Instruments Act, Cap. 2A, the Commissioner General on behalf of the Cabinet Secretary, National Treasury and Economic Planning, has developed the following Rules:

- Draft Income Tax (Pay As You Earn) Rules, 2024
- Draft Income Tax (Advance Tax) Rules, 2024
- Draft Income Tax (Withholding Tax) Rules, 2024
- Draft Income Tax (Guidelines on Allowability of Bad Debts Guidelines), 2024
- Draft Income Tax (Retirement Benefit) Rules, 2024
- Draft Income Tax (National Social Security Fund) (Exemption) Rules, 2024
- Draft Tax Procedures (Distraint) Rules 2024
- Draft Income Tax (Leasing) Rules, 2024
- Draft Income Tax (Registered Collective Investment Schemes) Rules, 2024
- Draft Income Tax - Declarations of Crops
- Draft Income Tax - Prescribed Limit of Medical Benefit.

In compliance with the same Act, the Commissioner General, on behalf of the Cabinet Secretary, the National Treasury and Economic Planning, invites interested members of the public, professionals and stakeholders to submit their inputs and comments for consideration in finalizing the Rules. The draft rules have been posted on the KRA website. You may download the draft rules for your reference.

Please channel your submissions to the Commissioner General, Kenya Revenue Authority, P.O Box 48240-00100, Nairobi or by email to [stakeholder.engagement@kra.go.ke](mailto:stakeholder.engagement@kra.go.ke) to be received on or before 22<sup>nd</sup> November, 2024.

Commissioner General  
Thank you for paying your taxes!

[www.kra.go.ke](http://www.kra.go.ke)

Disclaimer: KRA notifies taxpayers that it will not accept responsibility for payments not received, credited and validated in the relevant KRA accounts. **Corruption Reporting:** +254 (0726) 984 668. Email: [corruptionreporting@kra.go.ke](mailto:corruptionreporting@kra.go.ke). **Short Messaging Services (SMS):** Dial (\*572#) or Text to 22572. Contact Centre: +254 (020) 4 999 999, +254 (0711) 099 999, Email: [callcentre@kra.go.ke](mailto:callcentre@kra.go.ke). **Complaints & Information Centre Hotlines:** +254 709 017 700 / 800 Email: [cic@kra.go.ke](mailto:cic@kra.go.ke)



KENYA URBAN ROADS AUTHORITY

Transforming Urban Mobility



## TENDER NOTICE

This is to bring to the attention of the general public that an invitation for the following tenders has been uploaded on the **PUBLIC PROCUREMENT INFORMATION PORTAL and KENYA URBAN ROADS AUTHORITY'S WEBSITE**.

| No. | Tender Name                                                                                                                                                                                                                                            | Tender Number             |
|-----|--------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|---------------------------|
| 1   | The Road Annuity Programme Lot 15<br>Consultancy Services for Supervision of the Development of 2,000 Km of Roads Supporting Primary Growth Sectors Through Contractor Facilitated Financing Mechanism (Phase 1), Lot 15 Operation & Maintenance Phase | KURA/DEV/HQ/390/2024-2025 |
| 2   | The Road Annuity Programme Lot 18<br>Consultancy Services for Supervision of the Development of 2,000 Km of Roads Supporting Primary Growth Sectors Through Contractor Facilitated Financing Mechanism (Phase 1), Lot 18 Operation & Maintenance Phase | KURA/DEV/HQ/391/2024-2025 |

Bidders are requested to visit KURA's Website at [www.kura.go.ke](http://www.kura.go.ke) and [www.tenders.go.ke](http://www.tenders.go.ke) for more information.

Deputy Director – (SCM)  
For: DIRECTOR GENERAL



Kenya Urban Roads Authority



The Authority is ISO 9001:2015 certified



# Mashirika 8 ya Kijamii Lugari yapata vifaa vya kukausha mazao

NA MELECHEZEDECK EJAKAIT, KNA

